


Na Mhubiri wa Kimataifa Lamarck Lister

# KUOKOKA KWA WATU WA KIMAITA

Mark 16:14-18

# SHUKRANI

Namshukuru Yesu kwa kuniwezesha kutoa toleo hili la kwanza la kitabu cha KUOKOKA KWA WATU WA KIMAITAIFA. Kitabu hiki namtolea Yesu na Baba yake mapenzi yake yatimie kwa walioitwa na Yesu kuwa wahubiri. Awanurukishie akili zao zipate uelewa au ufahamu juu ya kusudi lake ktk maisha yao. Asante Baba wa Yesu na Yesu pia. Amen.

**MHUBIRIWA KIMATAIFA MINISTRY, FIRST EDITION 2024**

ISBN: 1986 - 08 - 08 - 01

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki hakiruhusiwi ku-nakili, kutafsiri au kuchapishwa kwa njia yoyote bila ru-husa ya Mhubiri wa Kimataifa ministry au Mhubiri wa Kimataifa Lameck Lister. Nakuu zote zimetoka ktk bib-lia (Maandiko matakatifu in Swahili Union Version)

**MHUBIRI WA KIMATAIFA MINISTRY.**

ADDRESS: S.L.P 9332, DAR ES SALAAM

TANZANIA (EFATHA)

MOBILE: +255658601034

EMAIL: listlameck5@gmail.com

KITABU KWA WALIOKOKA WANA WA MUNGU WAFANYAKAZI WA KIMATAIFA

1.Maana kuokoka …………………………………………………..

2. Yale mungu ametenda kwako …………………………..

3. Roho Mtakatifu……………………………………………….

4. Ushirika(Maono,Maombi,Sauti ya Mungu n.k)

5. Mamlaka uliyopewa na Mungu ………………………

6. Baraka …………………………………………………………..

7. Wewe ni nani mbele za mungu na ndani ya kanisa? Yesu amekuokoa Kwa kusudi lipi?

8.Ubatizo wa maji mengi……………………………………

9.Ufalme wa mungu…………………………………………

10.Karama au kipawa………………………………………..

11.Nuru imeingia ktk maisha yako………………………

12.Msaidizi ……………………………………………………..

13.Mwana wa Mungu……………………………

14.Upo mbinguni………………………………………….

15. Mwisho……………………………………………………

# 1. MAANA YA KUOKOKA

Kuokoka ni kuokolewa kutoka ktk maisha ya dhambi na kupewa na mungu kwa neema yake maisha ya haki ya mwanaye yesu. Mfano maisha ya dhambi yale uliyoishi kabla ya kuokoka maisha ya kuzivunja amri za mungu na sheria zake kama kuzini(kunaswa na wanawake wenye mitego ), kutoshika sabato, kuiba (ofisi kwa wafanyakazi wa kimataifa), ufisadi , rushwa, anasa(disko, ulevi) ,kuabudu miungu migeni (sanamu zilizotengenezwa kwa madini ya fedha,silver au dhahabu, michanga ya rangi ),dhuluma(mizani ya adaha),Ushirikina(kwa waganga wakienyeji), uchawi,mizimu, Kutamani wake jirani yako hata rafiki yako na kuzini nao, maisha ya kutamani mali za wengine na kuiba(ujambazi), Maisha ya Kutokujali wazazi au mzazi wako pengine ukilewa unamtukana na kumpiga au humpi mahitaji muhimu hata miaka ipite saba humnunulii hata kiatu n.k Mfano wa maisha ya haki ya yesu ni yale ya kulitendea kazi neno lake yesu.Haya ndiyo uliyoitiwa.Baadhi ya maneno ya yesu yanapatikana ktk vibabu vya injili ya mathayo, marko, luka na yohana. Na hayo maneno ndiyo kweli hukuweka huru mbali na dhambi kama yesu na husababisha nguvu za mungu kudhirishwa kwenye maisha yako ukijizoeza kuyatendea kazi. Maisha ya haki yakutakutaka uchukie maisha yako ya kale ya dhambi usitumkie dhambi tena na maisha mapya uliyopewa na mungu yatakupelekea kufanana na yesu kwa kuyatenda ya yesu kuhubiria watu wenye dhambi kama yesu , kuombea watu, kufundisha watu wenye dhambi ufalme wa mungu, kuponya wa walio wadhaifu na mungu na yesu

## 2.YALE MUNGU AMETENDA KWAKO

Ewe uliyeokoka ufanyaye kazi kimataifa kama za mashule ya kimataifa (mfano ualimu,ulinzi & upishi) upendwae sana na mungu(Baba) na mwanaye Yesu aliyofanya mungu ndani yako ni mengi sana tena mazuri yenye uzima kwako.

- Amekuisha kutoka kumilikiwa na nguvu za giza ndizo hasa asili ya dhambi na kukuingiza ktk ufalme wa mungu wenye asili ya haki.
- Amekupa msaidizi Roho mtakatifu ndiyo Roho yake hasa Mungu mungu aliyeumba mwili wako ikae ndani yako wajibu wako ni kuitii bila maswali. Na huyo roho amekuzawadia karama ukizifahamu na kuzitumia kwa kanisa utapata Baraka ya yesu.
- Amekusamehe na kukuondolea dhambi zako Kwa damu ya yesu iliyomwagika msalabani wewe ni mali ya mungu sasa na mwana wa agano.
- Amekupa mamlaka ya kuwaondolea wengine dhambi, kutoa pepo na kuponya wagonjwa.
- Roho yako ameiketisha mkono wa kuume wake Yesu ktk ulimwengu wa roho (mbinguni) mwili wako upo duniani.
- Amekuveka heshima, Baraka, Uweza na utajiri.
- Amekuokoa na hukumu kwa kukupa neema ya kumwamini mwanaye yesu.
- Amekupa ufalme wa mungu ndani yako utautambuaje (ishara) kuna badiliko la kiroho limetokea ndani yako unajiona kuna Amani isiyo ya kawaida ktk ndani yako au ktk maisha yako hiyo amani ilitoka kwa yesu baada ya kufufuka kwake, kuna furaha isiyo ya kawaida ktk maisha yako au ndani yako asili yake ni yale aliyotenda yesu na mungu ndani yako baada ya kuokoka na upendo wa mungu

## 3. ROHO MTAKATIFU

Huyu ni msaidizi amekupa yesu na baba yake akitoa msaada ktk maeneo yafuatayo

- Kukufundisha na kukumbusha yote yatokayo kwa yesu
- Kumshuhudia yesu ndani yako au ktk maisha yako.
- Kuwahakikishia ulimwengu juu ya haki dhambi na hukukumu.
- Kukuongoza ktk kweli (Kweli ni neno la Baba yake Yesu)
- Kukushauri ushauri utokao kwa yesu na kukupasha habari ya mambo yajayo.

## 4. Ushirika

Ushirika wako na mungu aliupoteza adamu kwa sababu ya dhambi wa kuzungumza na mungu hata nawe ukaliwa ktk hali ya dhambi sasa umerejeshwa baada ya kuokoka mungu anaweza kushirikiana nawe ktk njia zifuatazo na mkapatana au kuelewana:

## 4. MAOMBI

Kuanzia sasa tangu ulipookoka una kibali cha kuomba  jambo lolote jema unalohitaji na Baba wa mbinguni atakutendea.Hivyo unaweza shi-rikiana na mungu na kuzungumza naye kwa maombi.

- Maono - Mungu anaweza kushiriana nawe kwa maono yaani anaweza kutuma malaika wake wakuletee ujumbe wake au yesu na ukamwona na ukawaona au anapolala usiku akasema nawe kwa kukuonesha jambo analotaka akutendee na likatukia. Njia hii ya usharika mungu huitumia hasa kwa vijana.
- Ndoto - Wewe uliyekokoka unamilikiwa na yesu ndoto unazoota hutoka kwa mungu na yesu. Mungu anaweza kukupa ujumbe wake kwa njia ya ndoto. Njia hii ya ushirika mungu hutumia hasa kwa wazee.

## 4. SAUTI YA MUNGU

Unaweza sikia sauti ndani yako au nje iliyobeba neema ya uaminisho yenye upole, Amani yenye pumzi au mvumo kama wa upepo wa pentecoste, yenye msukumo(upendo wa mungu) ibeba habari njema za Yesu muda si mrefu hudhihirishwa.

- Maandiko - Roho mtakatifu atakufundisha yatokayo kwa yesu kwa njia ya maandiko na hiyo ni njia ya mungu kushirikiana nawe kwa kukupatia ya kwake
- Mtumishi wa mungu aliyetumwa na Yesu au Mungu (mitume,nabii,Mwalimu,Mwinjilisti,Mchungaji). - Mungu anaweza kushiriana nawe na kusema
- Nawe kupitia watumishi wake aliowatuma na kukupatia kile alichokuandalia kwa kukutendea matendo makuu na kukufikisha ufahamu wa cheo cha kristo.

## 5. MAMLAKA ULIYOPEWA NA MUNGU

Yesu Mamlaka uliyeokoka mfanyakazi ktk Nyanja mbali mbali za kimataifa kuziharibu kazi za shetani kama mapepo, magonjwa na nguvu zingine za giza kama uchawi.

6. Baraka

Mungu amekubariki kwa Baraka zote za rohoni kwa ndani yake kristo. Ili zidhirishhwe ktk ulimwengu wa mwili yesu ndiye njia ya kuzifikia. Unataka kuziona zilizo ndani yako yako yesu alisema ombeni lolote kwa jina la ngu nanyi mtapewa. Ombea bishara yako unayoimiliki baraka aliyokupa mungu ulipookoka idhihirishwe nawe utaona.

7. WEWE NI NANI MBELE ZA MUNGU NA NDANI YA KANISA? YESU AMEKUOKOA KWA KUSUDI LIPI?

- Tangu sasa ulipookoka mwana na mrithi mbele za mungu , mungu ni baba yako unaweza omba lolote likiwa sawa na matakwa yake akakupa baba wa mbinguni ukimwombwa urithi wa nyumba anakupa uwe na mahali pa kulaza kichwa imeandikwa baba mwema huwaachia watoto wake urithi wa nyumba na yesu anasema hakuna mwema ila baba peke yake yaani baba wa mbinguni ambaye ndiye mungu wetu aliyetuumba baba wa kimwili aliyekuzaa akukuachia nyumba mtoto kama urithi maamdiko humwita mwema si zaidi baba wa mbinguni hatazidi kuwapaurithi wa nyumba wale waliokokoka wamwombao na kufanyakazi ya mikono kwa bidii wakitafuta.

7. Uliyekooka mfanyakazi ktk Nyanja mbalimbali za kimataifa kama lubani ktk mashirika mbalimbali ya kimataifa ufahamu Yesu ana kusudi la kukuokoa na amekuita umtumikie kwa kazi yake ktk ufalme wa mungu na kanisa. Tangu sasa jifunze kufunga kuomba na kumuuliza Yesu umeniokoa kwa kusudi gani? Na kwa kazi  gani yako?

8.Ubatizo wa maji mengi

Neno “ubatizo” lina maana kutoswa au kuzamishwa ndani ya maji mengi . Yesu alitoswa au kuzamishwa ktk mto Yordani alipobatizwa na Yohana mbatizaji  kama umeamua kuokoka ubatizo wa maji mengi ni wa lazima kwako ili ufanane na Yesu ktk kubatizwa kwake. Ukweli utaupata kanisani au ktk huduma za waliokoka na hata mafundisho Yake uyapokee.

## 9. UFALME WA MUNGU

Ufalme wa ni utawala mungu wenye enzi,nguvu na mamlaka kupita tawala zote ktk ulimwengu wa roho hata zile zinazotawala ktk ulimwengu wa mwili yaani dunia.

Ufalme huu unatawala mbinguni kwa mungu kwa 100% kwa malaika na viumbe vya mbinguni pia kwa wana wa mungu wanawakilishwa na yesu ni mfalme hawa ni watakatifu walio mbinguni na waliookoka waliomo ktk dunia hivyo kama umeokoka mtu wa kimataifa na wewe umo hapo.

Mungu ambaye ni baba yake Yesu ndiye mfalme wa ufalme wa mungu wote ila sehemu ya ufalme wake amempa Yesu awe mfalme kwa waliokoka na watakatifu walio mbinguni.

Ufalme wa mungu ni wa haki, Amani na upendo **Rum 14 :17**

**"Maana ufalme wa Mungu si kula wala kunywa, bali ni haki na amani na furaha katika Roho Mtakatifu."**

Ulipookoka ufalme huu uliingia ndani yako. Roho mtakatifu alikujazi Haki ,Furaha,Amani na Upendo ni matunda yanayotambulisha u ndani yako. Kama ukuziona hizo isbara bora uombe mbele za baba wa mbinguni azidhihisbe ndani yako zina faida kwako .

Dalili za ufalme wa mungu kwenye mahali ulipo utaona miujiza inatendeka, wagonjwa wakiponywa, wenye mapepo na nguvu za giza wakitolewa, wakokokao wakijazwa nguvu za mungu na kuongea kwa lugha za malaika **Matendo: 2**

Maskini wakibarikiwa na kutajirishwa ktk Bwana Yesu.

Na wewe uliyeokoka mtu wa kimataifa Yesu aweza kukutua kwa hayo.

## 9. UFALME WA MUNGU

Faida ya matunda ya roho mtakatifu ktk maisha yaani amani,furaha,haki na upendo wa mungu.

- **Furaha**

Furaha ya mbinguni isiyo yanamna kidunia kufurika ndani yako. Furaha hii uliyoipata siku ya kwanza ya kuokoka ewe mtu wa kimataifa ni matokeo ya kutendewa mema na Mungu kama vile kusamehewa na kuondolewa dhambi kwa damu yesu , kuzaliwa mbinguni,kujazwa roho mtakatifu, kuhamishwa kutoka kumilikiwa na nguvu za giza na kuingizwa ktk ufalme wa mungu, kuondolewa hukumu /kufutiwa hatia ya dhambi ,kubarikiwa n.k. Kutunza hiyo furaha mungu anaka umwombe kila wakati mahitaji yako naye atakutendea amekuita akutendee mambo makuu apate kukufurahisha.

**Yoh 16.24**

**“Hata sasa hamkuomba neno kwa jina langu; ombeni, nanyi mtapata; furaha yenu iwe timilifu.”**

- **Amani**

Amani ya ufufuo wa Yesu uliyoipata na kuishuhudia siku ulipookoka ina maana gani kwako uliyeokoka mtu wa kimataifa? Umepatanishwa na Baba yake Yesu. Badiliko hilo la kiroho mtu wa kimataifa hutokea ndani yako kufumba na kufumbua unapookoka au ulipookoka ni amani ya kristo ndani ya moyo isiyo ya namna ya dunia au ulimwengu huu. Ukiifuata hiyo amani ya kristo kwa kuangalia ktk kila tendo ulitendalo kila siku huwezi tenda dhambi.

## 9.UFALME WA MUNGU

- **Upendo**

Upendo wa mungu huingia ndani yako na ktk maisha yako siku ile ulipookoka au unapookoka mtu wa kimataifa.Hujidhihiri ktk maisha hukuta kuyatenda ya mungu bila kusukumwa unajikuta baada tu ya kuokoka ukikutana mtu mwenye pepo unamtoa, mgonjwa unamwombea, hukusukuma kwenda ibada na kuyapenda  mambo ya mungu mengine kwa kuyashika na kuyatendea kazi bila kusukumwa ambayo mengine pengine kabla hujaokoka ulikuwa unayachukia. Dalili ya upendo wa mungu kufanya kazi ndani yako ni kutenda ya mungu au kufanyazi pamoja na mungu kama kushudia au kuhubiria watu.

- **Haki**

Yesu amekuveka haki yake ili usitende dhambi siku ile ulipookoka au unapookoka ewe mtu wa kimataifa. Jifunze kuishi maisha ya haki ya ufame wa Mungu kwa kutii Amani ya kristo na neno lake unalolipata kupitia watumishi wa Yesu yaani aliowatuma. Maisha ya zamani ya dhambi yaone kama mavi achana nayo jifunze hayo mapya kwa bidii na uhodari mwingi kama siku za ujana wako ulipojifunza maisha ya dhambi hukuzaliwa mlevi ulijifunza. Geuka kwa bidii jifunze ya haki kama vile utoaji(10%),kuomba,kutafakari biblia na kutendea kazi.Itii Amani ya kristo iliyo ndani yako nawe utakuwa na tunda la haki **Yakobo 3:18**

**“ Na tunda la haki hupandwa katika amani na wale wafanyao amani.”**

## 10. KARAMA AU VIPAWA VYA ROHO MTAKATIFU

Ishara au dalili kuwa umejazwa roho mtakatifu au umebatizwa kwa roho mtakatifu na yesu ni udhihiriko ndani yako au ktk maisha yako wa karama au vipawa vya roho mtakatifu. Udhihiriko huo hujitokeza siku ile ulipookoka au siku chache baaada ya kuokoka mtu wa kimataifa. Karama/ vipawa ni:

- **Kunena kwa lugha**

**Matendo 2;** Ishara karama ya kunena kwa lugha aidha za malaika au wanadamu huweza kujidhihirisha pindi unapookoka au ulipookoka ewe mtu wa kimataifa au siku chache baadaye.

- **Unabii**

**1samwel: 10: 1,5-6** Ishara ya karama ya unabii hujidhirisha kwa kutabiri Ulipookoka au unapookoka mtu wa kimataifa siku ile ile au baada ya siku chache.

- **Hekima**

**1samwel: 10: 1,5-6** Ishara ya karama ya hekima hujidhirisha kwa machozi ya furaha Ulipookoka au unapookoka mtu wa kimataifa siku ile ile.

- **Karama zingine** ishara zake hudhihirika siku chache baada ya kuokoka kama vile miujiza,uponyaji,kupambanua,neno la maarifa.na zinginezo hukutambulisha umejazwa roho na huleta mabadiliko ndani ya roho.
- Ukiitambua karama yako mwone mchungaji wako, mlezi au baba yako wa kiroho mwamie ili akuongoze na kukushauri.

## 11. NURU IMEINGIA MAISHANI MWAKO

Ukweli ewe mtu wa kimataifa uliyeokoka maisha yako yamejaa nuru kwa sababu huyo Yesu uliyempokea ndiye nuru. Maisha yako hayana giza tena uovu umeondolewa.

**Yohana 8.12**

**“ Basi Yesu akawaambia tena akasema, Mimi ndimi nuru ya ulimwengu, yeye anifuataye hatakwenda gizani kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima.”**

Maisha yako yana nuru ya uzima unapaswa kumfuata yesu kwa kutii neno lake. Baadhi ya maneno aliyosema Yesu yamo ktk vitabu vinne vya injili ktk biblia navyo mathayo,luka,marko na Yohana. Penda kusoma na kutafakari mema yaliyomo ktk maandiko ya vitabu hivyo vya injili na uyatendee kazi utapata Imani ya kweli ya Yesu yenye msingi imara.

**1Yoh: 1.5 — 7**

“Na hii ndiyo habari tuliyoisikia kwake, na kuihubiri kwenu, ya kwamba Mungu ni nuru, wala giza lo lote hamna ndani yake.

Tukisema ya kwamba twashirikiana naye, tena tukienenda gizani, twasema uongo, wala hatuifanyi iliyo kweli;

bali tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote”

Tunza hiyo nuru kwa kushirikiana Roho mtakatifu ktk kutenda yaliyo haki pachoni pa mungu wa mbinguni baba yake Yesu. Usiifiche iweke wazi yaani tangaza wokovu wako kwa matendo na maneno. Luk 8:16

## 12. MSAIDIZI

Msaidizi wako ewe uliyeokoka mtu wa kimataifa ktk maisha yako ya wokovu ni Roho mtakatifu. Huyu ulimpokea pindi ulipookoka ya siku ile ulipookoka au kubatizwa kwa roho mtakatifu.

Roho mtakatifu aliye ndani yako anatoa usaidizi ktk mambo yafuatayo:

- Kukufundisha na kukumbusha yote yatokayo kwa yesu.

Kukufundisha biblia ukimwombwa andiko lilio ktk injili akufundishe usiloliewa atakufundisha.

- Kumshuhudia Yesu ndani yako

Roho mtakatifu humshuhudia yesu ktk maisha yako kwa kukutendea makuu ya Yesu na kukutumia kuwatendea wengine makuu. Mfano kutoa pepo au kuponya.

- Kuhakikishi ulimwengu juu dhambi,haki na hukumu

Ukienda kuhubiri wenye dhambi roho mtakatifu aliye ndani yako huta sana huo usaidizi akishirikiana nawe. Kuwa Yesu ndiye mwenye haki , wanadamu wote wametenda dhambi, upo moto wa jehanamu kwa watakaokataa kuokoka kwa jina Yesu.

- Kukuongoza ktk kweli

Roho mtakatifu anakusaidia kukuongoza utii maneno ya mungu ktk yale unayotenda ya kila siku.

- Kukushauri ushauri utokao kwa Yesu ktk yale unayopitia
- Kukupasha habari juu ya mambo yajayo yatokayo kwa Yesu.

Mambo mema ambayo Yesu amekuandalia roho mtakatifu hukupasha habari ktk maono,sauti ya ndani ya roho yako,kupitia watumishi wa mungu.

13. UPO MBINGUNI

Kuokoka ni kuzaliwa mara pili mbinguni kwa maji na kwa roho; ni kutubu, kubatizwa kwa maji mengi na kujazwa roho mtakatifu.Yoh 3 : 5 — 7

**“Yesu akajibu, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu.**

**Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho.**

**Usistaajabu kwa kuwa nilikuambia, Hamna budi kuzaliwa mara ya pili.”**

Roho imezaliwa upya kwa njia ya Roho mtakatifu kama mtoto alivyozaliwa duniani na mwili ndivyo ulivyozaliwa ktk roho mbinguni mbele za mungu.

**Luk 10.20**

**“Lakini, msifurahi kwa vile pepo wanavyowatii; bali furahini kwa sababu majina yenu yameandikwa mbinguni.”**

Upo mbinguni tangu uokoke mtu wa kimataifa jina lako lime-andikwa kule baada ya kupewa wenyeji wa kule mbinguni una mamlaka dhidi ya pepo wachafu

**Marko 16:14-18**

“..**Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya;..”**

Roho yako uliyeokoka mtu wa kimataifa ipo mbinguni bali mwili wako kwenye dunia, roho yako ipo kule ili ipokee ya mbinguni yanayotakiwa kuzidhirika ktk dunia sawa

**Mathayo 6:10“Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni.”**

## 14. MWANA WA MUNGU

Mtu wa kimataifa uliyeokoka wewe ni umpewa uwezo wa kuwa mwana wa mungu umepewa haki kama ya Yesu mbele za mungu yakutwaa urithi wake alipewa na ulioshuhudiwa ktk maisha yake ya kwenye dunia kwa sehemu ya kutumiwa na mungu ktk kutenda makuu na kuishi bila kutenda dhambi.

**Yohana 1:12**

**“Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake;”**

**Wagalatia 4.6 - 7**

**“Na kwa kuwa ninyi mmekuwa wana, Mungu alimtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu, aliaye, Aba, yaani, Baba.**

**Kama ni hivyo, wewe si mtumwa tena bali u mwana; na kama u mwana, basi, u mrithi kwa Mungu.”**

Mtu wa kimataifa uliyeokoka umefanyika mwana roho mtakatifu uliyepewa tafuta mafundisho yake na jifunze habari zake kimatendo kwa kuyatii mafundisho yake ili upate ufahamu juu ya msaidizi aliye ndani yako anavyowasiliana/shirikiana nawe ktk kutoa usaidizi upate kuwekwa huru dhidi ya dhambi na Yesu ili ufurahie wokovu wako ewe mtu wa kimataifa uliyeokoka.

**Waebr 12:6 “Maana yeye ambaye Bwana ampenda, humrudi, Naye humpiga kila mwana amkubaliye.”**

Kwa kuwa u mwana Mtu wa kimataifa uliyeokoka epuka/kataa kufanya makossa/dhambi kuna fimbo kutoka kwa Yesu asije akakupiga kwa kufanya dhambi wokovu wako ukawa huna furaha.Mtoto ana haki ya kupigwa fimbo akifanya kosa apate kujirekebisha

# 15. KUOKOKA

Kama hujaokoka ewe mtu wa kimataifa na unataka kuokoka kiri maneno yafuatayo kwa kinywa chako kwa Imani Sema,

"Bwana yesu ninakuja kwako mimi ni mwenye dhambi natubu naamini ya kwamba ulisulubiwa kwa ajili ya dhambi zangu na laana zake damu yako ilimwagika nipate ondoleo la dhambi na kupatanishwa na baba yako na ulipigwa nipate ondolewa dhambi zangu, nisamehe dhambi zangu na uniondolee bila kusahau laana zake na ulifufuka nipewe maisha mapya huru mbali na dhambi na laana zake yaani maisha ya haki na baraka Yesu ingia ktk maisha yangu na ufalme wa mungu pamoja na roho mtakatifu unipe maisha hayo ya haki yako na baraka zake pia.Andika jina langu mbinguni nijaze furaha yako ya kunisamehe na kuniondolea dhambi na laana yake na kufanyika mwana mbinguni na kupewa sehemu ya urithi wako wa kutembea na nguvu na mamlaka ya mungu wako ya kuzivunja na kuziharibu kazi za shetani ikiwepo mapepo,magonjwa n.k. Asante yesu kwa kuniokoa , kwa roho mtakatifu, kwa neema yako, kwa karama au vipawa vyako, mamlaka yako, ufalme wako na nuru yako maana umeyafanya maisha yangu kuwa na uzima wako ... Amen"

Sasa umeokoka tafuta kanisa au huduma ya waliokoka na ushirikiane nao ili upate kukua hata kufikia ufahamu wa cheo cha kristo yaliyo ktk nchi yako au bara lako lakini kama upo Tanzania karibu efatha church yapo makanisa au huduma zingine za waliokoka au Ben Hinny ministry kama upo Marekani ; Paula white ministry n.k Yesu akuongoze kwa Roho wake mtakatifu kukupeleka ktk kanisa au huduma ya waliokoka ambayo utakuwa kufikia ufahamu wa cheo cha kristo ili Yesu akutumie sawa na kusudi lake la kukuokoa.

## 16. MWISHO

Kitabu cha kuokoka kwa **mtu wa kimataifa** kipo kukupa ufahamu wa yesu uliyempokea alichokutendea yeye na Baba yake wa mbinguni mpende kwa kulitii neno lake mfano **mafundisho yake** na **nabii zake .**

Mungu alikuokoa ee mtu wa kimataifa kwa njia ya Yesu kwa kusudi uishi naye kwa njia ya Roho wake mtakatifu ufanye mapenzi yake na mwisho ufike kwake baada ya maisha yako ktk dunia.Yesu amekuandalia mahali pa kuishi nawe ndio makao matakatifu

**Yoh 14:2-3**

**" Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo, ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi mwepo."**

Wewe uliyeokoka mtu wa kimataifa mwenye tumaini la kufufuliwa na Yesu ukifa leo je wajua unakiwa ufike ktk makao mahali alipokuandalia Yesu mbinguni ? Je pakoje? Tafuta na ununue Kitabu kilichoandikwa na Mwandishi aliyetumwa na Yesu kiitwacho **Kweli Mbingu Ipo?** Ukisome ufahamu Bwana Yesu alipokuandalia Baada ya Maisha Haya ukifa usipofika ufahamu hujafika.

Ukitaka kuwasiliana na Mtumishi ya Yesu Mhubiri wa kimataifa Lameck Lister :


**Tovuti:** www.mhubiriwakimaifa.org

**Baruapepe:** listlameck5@gmail.com

**Simu:** +2550658601034 or 0658601034

**Sanduku la Barua:** Efatha Church: P.o Box 3566 Mwenge DSM TZ



Mhubiri wa kimataifa Lameck Lister niliokoka mwaka 2003 kwa kuongozwa sala ya kuokoka na Paul Roberty nilipokuwa kidato cha Tatu Kibaha Sekondari nikiwa na umri wa miaka 17 ndipo nilipoupokea ufalme wa mungu.

**Mafundisho ya kukulia wokovu na Ubatizo wa maji mengi**

Mafundisho ya kukulia wokovu na ubatizo niliyapata ktk kanisa la Efatha mwaka 2003-2006. Yanahusu maisha mapya ya mtu aliyeokoka anavyotakiwa kuishi na ubatizo wa kristo. Ndani ya hayo mafundisho yanazungumzia maisha ya toba. tofauti ya maisha kabla hujaokoka na baada ya kuokoka na kile Yesu na baba yake amefanya ndani ya mtu aliyeokoka.

**Mafundisho ya Roho mtakatifu**

Mafundisho ya roho mtakatifu niliyapata mwaka 2007 ktk kanisa la Efatha - Mwenge DSM Tanzania. Na kuwekewa mkono na Mtume na Nabii Josephat . E. Mwingira mkuu na mwanzilishi wa kanisa la Efatha ili kujaa roho mtakatifu kwa upya na vipawa au karama kama ilivyo neema ya Mitume itokayo kwa Yesu kristo.

**Utumishi wa mungu**

Baada ya kumaliza mafundisho yote nimepewa cheti cha utumishi wa mungu cha ufahamu wa cheo cha kristo. Natambulikana ndani ya kanisa la Efatha kama Mtumishishi wa mungu mbele baba yake Yesu na Yesu kama mhubiri wa kimataifa. Ukitaka kuona cheti cha utumishi wa mungu nilichopata Ktk Kanisa la Efatha

Website:www.mhubiriwakimataifa.com

Email:listlameck5@gmail.com

Mobile: +255658601034 ; 0658601034